

HALMASHAURI YA MJI KAHAMA

(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Mkoa wa Shinyanga

Simu Nambari: 028-2710179

Fax Nambari: 028-2710179

e-mail:tcd.kahamatc@shinyanga.go.tz



Mkurugenzi wa Mji

S.L.P. 472,

KAHAMA

TAARIFA KWA UMMA KUKANUSHA TAARIFA ZA UPOTOSHAJI

Kumekuwepo na taarifa za uongo na upotoshaji zinazosambaa kwenye mitandao ya kijamii na majukwaa mengine ya habari yasiyo rasmi kuwa Hospitali ya Wilaya Kahama yakabiliwa na uhaba wa mashuka, blanketi na vyandarua hali inayowalazimu wagonjwa kubeba kutoka majumbani. Taarifa hizi ni za uongo na hazina ukweli wowote.

Ukweli ni kwamba Hospitali ya Mji Kahama haina uhaba wa Mashuka, blanketi na vyandarua na hakuna mgonjwa aliyekosa hadi kumlazimu kuja na vya nyumbani.

Tunaomba umma utambue kwamba taarifa tofauti na hizi ni taarifa za upotoshaji na ni kinyume cha sheria na maadili ya habari.

Kwa hatua nyingine Halmashauri ya Mji Kahama inaomba kituo cha Radio One Stereo cha Dar es Salaam ambacho kuitia ukurasa wake wa “twitter” wa “@RadioOneStereo” kilirusha taarifa hiyo (Kwa mujibu wa screenshot inayosambaa) kurekebisha taarifa yao.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read "Charles J. Mnyani".

Charles J. Mnyani

Afisa Habari na Mahusiano

Halmashauri ya Mji

KAHAMA

17th October, 2017